Lile Shindano

Njia Zake hazitafutiki, au sivyo? Bwana wa ajabu! Ni tamu vipi kumtumainia. Nina hakika mmekuwa na furaha usiku huu. Na nilipofungua tu mlango hapo muda mfupi uliopita na kusikia Dada Gertie akiimba huo wimbo wa zamani, *Endelea kushikilia, Saa Moja Zaidi Tu*. Ulileta ukumbusho wa kanisa langu dogo, hapo kabla sijakwenda katika kazi ya umisheni. Ninatazama, "Mtafute Mungu Kwanza" hapa katika ubao huu wa kale, nakumbuka Sammy Davidson alichora hapo hapa miaka ishirini na mitano iliyopita, upande ule mwingine nadhani kuna, "Utaishi wapi Milele? Waza"! Na papa *hapa* palikuwepo mwa—mwawanamke kisimani, na Danieli katika tundu la simba. Jamani! Mambo mengi yametendeka tangu wakati huo.

2 Yapata saa kumi na moja adhuhuri ya leo nilipata simu ya mtu hatarini iliyotoka yapata maili thelathini au arobaini hapa nchini, ya mwanamke aliyekuwa akifa, ni rafiki mpendwa sana, mama ya Georgie Carter. Nami nilijua kuwa kuna wahudumu wengi ambao wangeshikilia hadi nirudi. Edith pia amekuwa mgojwa sana. Na tulipokuwa huko, Bwana Mungu alijitokeza, na Dada Carter yuko mbali sana na kifo. Kwa hivyo, twashukuru kwa ajili ya hilo.

3 Na sasa unakaribia wakati wa ibada ya ushirika hivi punde, nami nadhani ni karibu saa sita watakapoanza. Mmeupa saa ipi? [Ndugu Neville asema, "Wakati wowote, kuanzia sasa hadi saa tano u nusu."—Mh.] Wakati wowote tu ambao tuta. . .Wangapi watakaopokea ushirika usiku huu, hebu tuone mikono yenu. Hilo ni, lo, hilo ni ajabu. Vema, nataka kunena neno moja au mawili. Labda nitaweka saa yangu hapa kwa dakika kama kumi na tano, tutaanza ushirika. Naam, mwampenda? Amina. Najua mmekuwa na wakati mkuu, sivyo?

4 Vema, ikiwa hapa hawako Ndugu Thomas Kidd, na Dada Kidd, toka huko Ohio. Nadhani wamekuja. Lo, hilo ni nzuri, nadhani liko kwenye kanda nami nitalipata. Mwajua, Wao hawavunjiki moyo. Wao wamebakisha siku chache tu wafikie miaka mia moja, lakini—lakini hilo ndilo hunipa moyo, ni kuona watu kama hao. Waza, mimi ni mzee, na kabla sijazaliwa wao walikuwa wakihubiri Injili. Na ndipo nipo hapa mzee, nao, ikiwa hawawezi kwenda nje na kupaza sauti zao, wao hupeleka chombo cha habari iliyonaswa na kwenda toka hospitali moja hadi nyingine, nyumba kwa nyumba, wakihubiri Injili. Hilo ni nzuri ajabu. Amina. Nawafurahia hakika na pia wao wote waliotumainia ibada hizi hapa.

5 Sasa, kumbuka, tutaitangaza saa, Bwana akipenda, mara tu kanisa likamilikapo, ambapo wanadai itakuwa kama Februari kumi hivi, na sisi, Bwana akipenda, twataka tuchukue siku zisizopungua nane ama kumi, au labda majuma mawili, kwa ajili ya hiyo *Mihuri Saba* ya Ufunuo. Na tutawatumia kadi wageni wetu wanaotoka hapa karibu, toka hapa nyumbani, na tutawajulisha mapema sana ili wakitaka kuhudhuria, vema, bila shaka tutafurahia kuwa nanyi hapa. Na pengine Bwana atatupa onyesho lingine la Uwepo Wake kama vile alivyofanya wakati uliopita tulipomaliza kuhubiri zile *Nyakati Saba za Kanisa*.

6 Unapotaka kumwombea mtu fulani naam, nikumbuke mimi kila mara, kwa sababu ni mimi ndiye ninayeyahitaji sana. Basi, mimi naona haya kuchukua hizi dakika kumi ama kumi nao hapa, kunena jambo fulani kidogo kabla hatujaanza, lakini hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi.

7 Bwana Yesu, lo, siku moja vita vitakwisha, na hapatakuwepo tena wagonjwa wa kuombewa, na hapatakuwako tena wenye dhambi wa kutubu. Lakini, Baba, wakati hii siku iko kama ilivyo, hebu tufanye kazi mradi tungali tuna nuru ya kufanyia kazi, kwa kuwa saa yaja ambapo hakuna mtu ataweza kufanya kazi. Sasa kwa dakika chache tu, Bwana, ningejisikia vibaya kama singefanya kazi, naliumaliza mwaka huu bila kusema maneno mengine machache. Nisaidie, Baba, naomba, ili niseme kitu fulani ambacho kingetia ujasiri mioyoni mwa watu Wako, ili tutokapo hapa usiku huu baada ya kupokea ushirika, nasi twatambua kuwa katika ushirika kuna nguvu. Israeli walipokea ushirika mara ya kwanza huko Misri, na kutembea miaka arobaini bila viatu vyao kuraruka au nguo zao kuchakaa. Na, kati ya watu milioni mbili, hapakuwa na ye yote mnyonge miongoni mwao walipotoka jangwani. Bwana, hebu tukumbuke hilo usiku huu tunapokaribia wakati huu mkuu. Twaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

8 Kama ningalihubiri somo ambalo nilikuwa nimeandika nililokuwa naenda kulianza adhuhuri hii, tungekuwa hapa hadi saa kumi na moja asubuhi. [Ndugu Neville asema. "Hilo lingekuwa jema."—Mh.] Lakini nataka kusoma tu Neno toka kwa . . . Asante. Toka kwa Waefeso, sura ya 6, kifungu cha 12, na kwa dakika chache sasa, kujipa moyo.

> *Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka juu ya . . . wakuu wa . . . giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.*

9 "Pepo wabaya katika ulimwengu wa roho." Nami ningependa kupata hapo somo dogo la dakika kumi ama kumi na tano, au fungu, samahani, nataka kuliita: *Shindano*. Shindano ni jaribio la nguvu. Nasi, ambao tuna . . . jaribio la nguvu. Tulikuwa na . . . Wahindi walikuwa wakiwasha moto,

nao wangeweka watu kiasi fulani upande huu wa kamba, na watu kiasi fulani upande *huu,* na m—mchezo wa kushindana kuvutana kwa kamba, kushindana nguvu, wangelikokota kundi lililoshindwa kupitia huo moto. Na sasa twajua kuna mambo mengi, nasi tungeweka haya juu yake kwa dakika chache, ya—ya kushindana, lakini nataka kunena kwa hizi dakika chache upesi kuhusu shindano kubwa lililoko, yaani, kati ya Kanisa na Shetani. Hizo nguvu kuu za Shetani. Nasi twataka kunena kuhusu nguvu kuu za Mungu katika Kanisa Lake.

10 Sasa, hili shindano kuu limekuwa likiendelea kwa miaka mingi. Lilianzia Mbinguni, na Shetani akatupiliwa mbali hata duniani, ndiposa yeye akawa adui kwa watu wa Mungu. Na, tangu hapo, yeye ametumia nguvu zake zote na hila zake kujaribu kuwavuta watu wa Mungu wapitie motoni, au, katika mioto yake.

11 Nasi twajua Yule aliye na guvu nyingi zaidi, Mungu anazo. Naye Mungu alipowapa watu Wake kitu kizuri zaidi ambacho angeweza kuwapa kushindana na Shetani, kilikuwa Neno Lake. Sasa, kwa sababu Neno ni Mungu, na ni nani aliye na nguvu kumshinda Mungu? Kwa hivyo, Neno ni Mungu, nalo ndilo nguvu zetu. Mungu katika Kanisa, huwa Nguvu zake za kumvutia Shetani aingie katika mioto yake mwenyewe aliyoitengeneza. Na kuvutana kwaendelea. Sasa, Yesu alisema, katika Marko 16, "Katika Jina Langu watatoa toa pepo."

12 Naam, najua huo ni msemo wa kale ambao watu. . .kuna msemo wa kale kuwa. . .Nao sio wa kale sana, hata hivyo. Watu hawaaamini katika pepo siku hizi. Lakini jambo la kufanya, nionavyo mimi, ni kumjua adui wako. Na—na mjue adui wako, na ujitayarishe kwa shindano ambalo utakuwa nalo mkutanapo, kwa sababu utakabiliana naye. Na umjue, ujue zake, ujue nguvu zake zilivyo, ndiposa ujizoeze kwa ajili ya hili shindano utakapokabiliana naye. Kwa kuwa kuna jambo moja dhahiri, utakabiliana naye. Na kwa hivyo ujizoeze kwa ajili ya shindano hilo.

13 Sasa, kujitayarisha kwa ajili ya shindano ni kama tu mwana ndondi. Adui wake—wake ambaye atakutana naye nje huko katika shindano, wapigane, mwana ndondi kweli kweli kila mara hujua na kumchunguza mpinzani wake. Yeye huchunguza kupigana kwake, ajua anakopenda kupiga makonde, kama huinama mbele, hujitupa nyuma, hupigana kwa mkono wa kulia ama kushoto. Yeye huchungunza haya yote. Na ndipo ikiwa yeye ni mpiganaji mzuri, mwerevu, yeye hujizoezea mwana ndondi mwenziwe ambaye atapigana kama tu mpinzani wake, kwa maana atajua kupigana kwake kwote afikapo mahali pale.

14 Nami nafikiri hilo ni jambo bora sana kwa Wakristo kufanya. Hilo ni nzuri. Na sasa kama wataka kuanza mazoezi, anza na Yohana 3:16, ile Amri kuu. Anzia papo hapo na hicho, nacho

kitakuingiza jukwaani. Na ndipo ujizoeze makonde ya mwisho, kwa sababu itakubidi kuyatumia. Kila mtu ajua hilo. Lazima upate mazoezi ya kumpiga adui wako. Na kila mara, Mungu hutumia Neno Lake. Lazima tukumbuke kuwa Mungu hutumia Neno Lake kumshinda adui Wake. Kama Mungu angeliwazia au angeliwapa watu Wake cho chote bora zaidi cha kumshinda adui, Yeye angelifanyia hivyo. Kwa hivyo kama nimekuwa nikisema kila mara, "Mungu akatapo shauri, hilo ndilo bora zaidi lililopo. Yeye hawezi kamwe kubadili shauri Lake." Kwa hivyo shauri la kwanza Mungu alilowapa watu Wake katika Bustani ya Edeni, kumshinda adui, lilikuwa Neno Lake. Walikingwa na Neno Lake.

15 Na sasa adui atachungunza . . . maarifa yetu ya kupigana kwa Neno. Naam, Shetani alijifunza hayo kikamilifu sana hata, alipomjia Hawa, yeye alikuwa na zile—zile hila nzuri sana za vita ambazo yeye angeweza kutumia amshinde, na hizo zilikuwa kuhojiana na Neno. Sasa, hauhitajiki kamwe kohojiana na Neno la Mungu. Liamini tu. Usijaribu kulifafanua. Usijaribu kuliwazia. Sasa, hauwezi kumwazia Mungu, kwa hivyo Mungu ni Neno, nalo limewekwa tu liaminiwe. Nalo ni Nguvu yetu, likubali tu Neno. Na kila mtu ajua mbegu katika ardhi bora itazaa ile ya aina yake. Basi lazima tulishike tu Neno.

16 Na, sasa, Hawa akaanza kusimama atoe hoja zake wakati yeye . . . yeye alipomnukulia Neno, "Mungu alisema, 'Usile, kwa maana siku utakapoula siku hiyo tutakufa."

17 Naye Shetani hakukataa aliyoyasema. Yeye alisema, "Bila shaka, hiyo ni kweli." Lakini yeye alisema, "Waona, wahitaji Nuru nyingine mpya." Kitu fulani tofauti kidogo na kile Mungu alichosema. "Na ukifanya hivyo, utakuwa mwerevu kidogo zaidi. Macho yako yatafunguliwa."

Lakini yeye alisema, "Vema, Mungu alisema tungelikufa."

18 Yeye alisema, "Ah, hakika . . . " Unaona, hapo unakuja, umbali huo tu, "Hakika hamtakufa." Lakini Mungu alisema mngekufa, na hilo latosha! Na hi—hilo likashinda hayo mashindano ya kuvutana kwa kamba wakati huo, na kuvuta uzao wote wa mwanadamu mautini, kwa sababu Hawa alisikiza hoja dhidi ya Neno la Mungu. Sasa, ni aibu kwamba alifanya hivyo, lakini yamepita. Bali sasa tungali tumekingwa, na huo upatanisho ulifanywa katika Kristo Yesu. Twajua hilo. Mungu alitupa kinga bora zaidi, kulitumaini tu Neno Lake.

19 Mwajua, na wengi wanasema siku hizi kuwa hakuna kitu kama Shetani. Wanaamini kuwa ni wazo tu. Wanaamini hilo. Na kuna watu wanaoamini hilo—kuwa—kuwa Roho Mtakatifu ni wazo nzuri, na eti Shetani ni wazo baya. Lakini ukichunguza, Biblia inaponena kuhusu Roho Mtakatifu, Yeye alisema, "Huyo roho mtakatufu ajapo". Na "huyo" Ni neno la kumtaja mtu. Unaona? Kwa hivyo, huyo, huyo ni nafsi. Na shetani ni nafsi.

Na pepo ni nafsi. Naam, hao ni pepo nao huja kwa njia nyingi. Lakini wao hudhani ni wazo la mtindo wa kale.

20 Mtu mmoja alikuwa akibishana nami majuma machache yaliyopita. Yeye alisema, "Wajua ufanyacho? Wewe huyafanya mawazo ya hao watu yawaze kitu fulani uwaambiapo kitu hicho. Ni badiliko la mawazo."

21 Nilikutana na jambo lile lile huko India wakati mmoja, wakati hao watu watakatifu walipokuwepo pale tulipokuwa na, naamini umati mkubwa niliowahi kuuhubiria, katika umati mmoja mkuu, wakiwamo watu nusu milioni, nami nililipata kwa upambanuzi katika Roho. Nao wangeona Roho Mtakatifu akiwaita watu, na kuwaita, kule, katika ule umati, na kuwaambia mambo mbali mbali, na kushika mawazo yao. Hao watawala wa Kihindi na watu watakatifu, walisema, "Yeye anasoma mawazo yao."

22 Kwa hivyo kwa muda mfupi, watu kama watano ama sita hivi walikuwa wamepita katika huo mstari wa maombi, na mtu aliyekuwa kipofu akaja. Naye alikuwa kipofu kabisa, na macho yake yalikuwa meupe kama hili shati langu. Nami nilisema, "Sasa hapa kuna kipofu, ye yote aweza kuona yeye yu kipofu." Tena nikasema, "Kama ningeliweza kumsaidia ningefanya hivyo, lakini njia tu ambayo ningemsaidia ni kupitia kwa kipawa, labda kwa kusema kitu fulani alichotenda; na hilo lingeleta wazo kuwa ikiwa Mungu ayajua yale huyu ametenda, Yeye bila shaka angejua kile atakachotenda." Kwa hivyo nilisema, "Sasa, nikimtazama yeye," nilisema, "sasa, yeye ni mwambudu jua. Amekuwa kwa miaka ishirini." Na, mkalimani alipoyanena, hayo yalikuwa sahihi. Nalisema, "Yeye ameoa. Yeye . . . mkewe ni mdogo, naye ana wana wawili, mmoja wa umri wa miaka saba hivi, na mwingine tisa." Hilo lilikuwa sahihi hasa. Nikayataja majina yao, yalivyokuwa.

23 Ndipo huko katika umati, watu walikokuwa, kukaja lile wimbi, "Ni mafikira, ni kitu fulani kama hicho cha—cha kusoma mawazo yao."

24 Ndipo nikawaza, "Bwana, ukinisaidia tu. Na—nahitaji msaada Wako, Bwana. Watu hawa wanalinganisha haya na uwezo wa kushirikiana mawazo. Nayo sivyo, Nawe wajua hivyo, Bwana." Hata sasa, ningewapa Maandiko ambayo Yesu alisema Yeye hakufanya cho chote hadi Baba Yake alipomwonyesha. Na ndipyo, nilipogeuka kumtazama mtu huyo tena, nikamwona yeye juu kidogo hapo katika ono, akiwa na macho mazuri tu kama nilivyo nayo. Nikawaza "Huu ndio wakati."

25 Nikasema, "Huyu mtu ni mwabudu jua, sasa, naye amekuwa kipofu." Tena nikasema, "Sasa, ile . . . kuna mashehe wa Mohammed, na kuna wale—wale maimamu wa Shiite, Jain, na dini aina mbali mbali, Budha. Mtu huyu sasa anataka aweze kuona tena. Sasa, mngesema kuwa yeye—yeye aliabudu kiumbe

badala ya Muumba. Naamini hilo pia. Lakini tumeketi hapa usiku huu.” Nilisema, “Nasi tumekuwa. . .leo nilikaribishwa katika hekalu la Jains amboko zilikuwemo dini mbali mbali kumi na saba kunihoji, nazo zote zikimpinga Kristo, kila moja!” Nami nilisema, “Sasa, nanyi wengi wenu mlikuwa huko. Sasa, ikiwa Kristo alikosea, basi mtu huyu ataka awe sawa, na bila shaka Mungu wa viumbe aliyeumba dunia atakuwa ndiye pekee atakayeweza kumfanya aone. Hilo ni nzuri,” Tena nikasema, sasa, ikiwa mmoja wenu enyi watu, Islamu hapa ndiyo dini kuu ya zote, ikiwa shehe wa Kiislamu aweza kuja hapa na kumfanya aone tena, basi nitafuata Uislamu, au ikiwa kasisi wa Ki—Buddha aweza kuja na kumfanya aone tena. Lakini hebu na yule Mungu aliyemuumba, yule Mungu, Mungu wa mtu fulani aliyeko mahali fulani, kwa sababu lazima aweko, hatuwezi kuwa na kiumbe pasipo kuwa Muumba. Naam, Muumba atahitajika aumbe kuona katika macho yake. Yeye amekuwa kipofu kwa miaka ishirini tokana na kutazama jua, akidhani atakwenda Mbinguni akifanya hivyo. Mtu huyu alifanya hayo kwa kutokuj ua.” Nilisema, “Je, ninyi makasisi wa Ki-Buddha mngefanyaje? Mngebadili tu njia yake ya kuwazia. Mngesema yeye amekosea.” Wao huwaabudu mizimu yao. Tena nilisema, “Sasa, mwadhania yeye alikuwa hivyo, mngesema yeye alikosea, lakini mngefanyaje? Mngebadili njia ya kuwaza kwake.” Nami nikasema, “Ninyi Waislamu mngefanyaje? Mngebadili njia ya kuwaza kwake. Wa-Shiite, Wa-Jains, na kadhalika hubadili njia ya kuwaza.”

26 Nilisema “Tuna kitu kama hicho Amerika. Wamethodisti wote wanataka kuwafanya Wabaptisti wote wawe Wamethodisti, nao Wapentekoste wanataka kuwachukua Wamethodisti wote na kuwafanya Wapentekoste. Ni badilisho la wazo. Lakini hilo silo tunalonena juu yake. Tunanena kuhusu Mungu, aliye Muumba.” Nami nikasema, “Hakika Muumbaji angenena.” Na, sasa, singesema hayo kama ono hilo halingekuwepo, hasha kwa vyo vyote. Sasa nilisema, “Sasa, ikiwa yule Mmoja, tumwache Yeye awe Munga, na aje ampe kuona kwake.” Tena nikasema, “Sasa namhimiza shehe ye yote au Mtawala, au mtu mtakatifu au mtu awaye yote, aje ampe kuona kwake, nami nitafuata filosofia yako, utakuwa umejipatia mfuasi.” Na hao walikuwa watu watulivu sana niliowahi kuwasikia. Mwaona? Hakuna ye yote aliyefanya hivyo.

27 Nami nikasema, “Mbona mmenyamaza sana hivyo?” Nikasema, “Sababu yake, ni kwa maana hamwezi kulifanya, wala hata nami pia. Lakini Mungu wa Mbinguni aliyemfufua Mwanawe Yesu Kristo, ambaye sisi tu watumishi Wake, sasa hivi amenionyesha ono kuwa mtu huyu atapokea kuona kwake.” Mwaona? Nilisema, “Sasa, ikiwa hiyo sivyo, basi mwaweza kunifukuza India. Lakini ikiwa ndivyo, kila mmoja wenu anapaswa kumpa Yesu Kristo maisha yake. Ningetaka

kuwaulizeni, ni wangapi walioko hapa watakaompa Kristo maisha yao ikiwa mtu huyu atapokea kuona kwake? Mwawaona makasisi wenu, hakuna ye yote anayekuja hapa. Mbona hawaji, ikiwa wamewaambia kuwa dini zao ni kubwa na kuu sana? Mbona mtu haji na kusema kitu fulani?" Hakuna ye yote aliyekuja. Nilisema, "Basi ninyi watu mlioko hapa nje, mkiona mtu huyu aliye kipofu anayesimama hapa . . . "

28 Na hapo daktari akaja na kuchunguza macho yake. Akatikisa kichwa chake, na kusema, "Yeye yu kipofu."

29 Na kwa hivyo nilisema, "Hakika, yeye yu kipofu." Lakini nilisema, "Ikiwa—na ikiwa Mungu atampa kuona kwake, ni wangapi wenu mtamtumikia Yesu Kristo?" Na kwa umbali nilioweza kuona bahari ya mikono myeusi. Nikamgeukia mtu huyo, na kusema, "Bwana Yesu, hebu na ijulikane kuwa Wewe ni Mungu." Mtu huyo akanikumbatia shingoni, na hapo alikuwepo meya wa mji wa Bombay ameketi pale, akamkumbatia shingoni, akiona vizuri kama mtu yeyote awezavyo kuona.

30 Ni nini? Ni—ni nguvu halisi! Mungu ni Mungu, na Shetani ni Shetani! Ikiwa hauamini Shetani . . . Nilipoanza kwanza, nili—nilikabiliana naye uso kwa uso kila siku. Usiniambie hakuna Shetani, kwa sababu najua vizuri zaidi. Yanilazimu kupigana naye kila siku. Kwa hivyo najua kuna—kuna Shetani. Na lazima upate mazoezi ukutanapo naye. Si mazoezi ya kusomea mawazo, si mazoezi ya elimu, lakini mazoezi ya Roho Mtakatifu. Nguvu za Mungu katika Neno Lake kulifanya lidhihirike. Mjue adui wako. Lo, yeye yu mkatili vipi!

31 Jinsi ningependa kusimama hapa sasa na kushikilia hilo, nirudi katika Biblia na kukuonyesha mtu huko nyuma aliyekutana nalo uso kwa uso. Jinsi katika shindano dhidi ya adui, walijikinga kwa Neno la Mungu. Nuhu alipata ujuzi wa hilo, naye alijua kuwa Mungu alimwambia itanyesha. Na shindano likawaka moto baina ya sayansi na Neno la Mungu: Sayansi yasema, "Haiwezi kunyesha." Mungu alisema, "Itanyesha." Amina.

32 Jambo kama hilo lipo sasa. Itatendeka! Hutendeka! Kuna pepo! Lakini Yesu aliwatoa, naye alilipa Kanisa Lake mamlaka ya kufanya hivyo, "Toeni pepo katika Jina Langu!" Yeye aliwatoa pepo saba, toka kwa mwanamke mrembo siku moja. Naye alisema, "pepo mchafu anapotoka kwa mtu, huyo hutembea katika mahali pakavu, akirudi tena basi, huja na pepo wengine saba pamoja naye." Sasa, hilo laonyesha kuwa ikiwa mtu huyo alitolewa pepo, kulikuwamo kitu fulani ndani yake kilichomtoka. Pepo alikuwa amemtoka! Sasa, pepo alipotoka, hapo Mungu . . . hilo lampa Mungu nafasi ya kuingia. Kwa hivyo, aondokapo, mruhusu Roho Mtakatifu kuingia. Usiachie tu hapo. Lakini ukitubu dhambi zako tu na kuendelea, ndipo utakuwa mbaya zaidi ya ulivyowahi kuwa. Lakini fanya mahali hapo

ambapo Shetani aliishi wakati mmoja na kupamiliki, pafanye pajazwe na Roho Mtakatifu wa Mungu, na ndipo utakuwa na nguvu za Neno la Mungu ndani yako, zimedhihirishwa, na ukatoe pepo. Shindano linaendelea. Nuru za jioni zinang'aa. Roho Mtakatifu wa Mungu yuko hapa.

33 Na sasa imebaki kama—karibu dakika tatu hivi hadi wakati ambapo filimbi zitapigwa, na itakuwa usiku wa manane. Ndipo tuondokapo katika jengo hili, tukienda mahali petu mbali—mbali na manyumbani mwetu, na kukutana nje; na kukabiliana na ulimwengu, na tusienende kama tulivyokuwa katika nyakati zilizopita. Hebu na tuenende katika nguvu za kufufuka Kwake. Na tuenende katika Jina la Yesu Kristo, tukiwa na bendera iliyoinuliwa juu, na tukiwa na imani katika Neno Lake, kushika huo Upanga ukatao kuwili, tukiwa na ngao na silaha zote za Mungu, kukabiliana na adui, kwa sababu yeye anajiimarisha na kuwa na nguvu kuu kila siku. Kama yule huyu adui anapokuj a kama mafuriko, Roho wa Mungu huinua beramu dhidi yake. Kama tumefika mwisho wa mambo haya ambayo sisi. . .na siri za Mungu zimetimizwa kwetu, twatarajia nguvu zaidi, nguvu za kunyakuliwa, kukabiliana na. . .nguvu mbaya zaidi, ambazo zitalinyakua kanisa na kulipeleka Utukufuni. Lazima tuwe nazo. Na tuingie katika mwaka wa '63 tukiwa na mwito wa mashindano, kama, sisi ni watumishi wa Mungu aishiye! Na kama Shadraka, Meshaeli na Abednego wa zamani, hatutasujudu pepo wa ulimwengu huu na kughairi vitu hivi tulivyonena kuvihusu, lakini hebu tujitahidi vitani.

34 Najisikia usiku wa leo tunapozisisiza hizo filimbi, kitu fulani kama Daudi alivyofanya usiku huo wenye joto na wa kuogofya alipolala hapo chini ya vichaka vya miforsadi, na adui wakamwamsha. Ulikuwa wakati wa jinsi gani kwa Daudi! Ni wakati wa jinsi gani yeye alipolala hapo! Yeye hakujua la kutenda, hakujua aende na nini, kwa sababu yeye alijua adui ni wengi. Lakini, papo hapo, akasikia kama sauti ya upepo ukipitia juu ya vile vichaka. Yeye alijua Mungu alimtangulia, naye akaenda vitani. Nasikia kitu kama hicho usiku huu, baada ya Ujumbe wa usiku uliopita, niko katika wakati wa giza sana niliowahi kuwa nao maishani mwangu. Najisikia kama Isaya hekaluni baada ya kuona hao malaika, mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu. Lakini sikizeni—mimi—mimi ni—lazima nikabiliane nayo siku moja, na, jambo ni kwamba, nangoja kusikia hiyo ikivuma katika vichaka vya miforsadi, kwenda kukabiliana na adui popote alipo. Mungu atusaidie kufanya hivyo.

35 Na sasa nadhani imebaki dakika moja kufika usiku wa manane. Na mwaka wa '62 pamoja na yake yote yanayopita, na yapite.

36 Na tusimame sasa, kila mmoja wetu. Shindano laendelea kila mmoja wenu. Paulo alisema, "Nikiyasahau yaliyo nyuma,"

makosa ya mwaka uliopita, “nakaza mwendo niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu.” Makosa yangu yote niliyoyatenda miaka hii yote, nisamehe hayo. Mungu, nisamehe. Kanisa, nisameheni. Na huduma ambayo nili—nilikosea kwayo, najisikia; Mungu, nisamehe hayo. Kanisa nisameheni makosa yangu. Nami nitakaza mwendo, niifikie mede ya thawabu ya mwito mkuu katika Kristo Yesu. Ya kesho siyajui, lakini namjua Yule aliye na ya mwaka wa 1963.

37 Hebu tuinue mikono yetu kwa Mungu sasa na tuombe tupendavyo, tunapoungama, na kumwomba Mungu atusaidie kote katika huu mwaka mpya ujao.

38 Baba wa Mbinguni, tunaposimama hapa, mawazo mengi yanapokufa mioyoni mwetu, na makosa yetu ya mwaka uliopita, na tunapokaribia kifo cha mwaka wa ’62 na kuzaliwa kwa mwaka wa ’63, Ee, Mungu, na tuwe hatua moja juu ngazini, hata tuweza kumwona Yesu na mpango Wake. Na kila mmoja hapa, Bwana, katika maombi, wakati mwaka mzee unapokufa, na kuzaliwa upya kwa mwaka mpya kunaingia, hebu dhambi za yule mtu wa kale na kutoamini zife mioyoni mwetu, na kuzaliwa upya kuingie pamoja na mwaka wa 1963, kama uvumi wa Upepo wa nguvu ukienda kasi, ambao waweza kuzijaza nafsi zetu na kutufanya viumbe vipya katika Kristo.

39 Utufanye watumishi wanaostahili. Tusamehe yaliyopita. Tubarikie ya usoni. Tuongoze, Ee Bwana Mungu, kwa mkono Wako wa nguvu, Yehova. Wabariki wahudumu hawa hapa. Bariki washiriki wote, wageni wote. Uwe pamoja nasi, Bwana. Sisi tu watumishi Wako, nasi twajitolea kabisa Kwako kwa huu mwaka wa 1963, nguvu za Roho Wako zitawale maishani mwetu na nafsini mwetu. Tusaidie, Mungu. Tusamehe na utusaidie, twaomba. Wainue watu hodari, wainue wanajeshi hodari wa Imani! Funua mwaka huu, Bwana, hiyo mana iliyofichwa, huo Mwamba ulio chini ya mwamba, ili tuweze kuuona mpango wa Mungu. Funika piramidi za maisha yetu, Bwana; weka jiwe la Kifuniko, Kristo Yesu, juu ya kila mmoja wetu. Na hizi baraka Zake kuu za ajabu takatifu, ziwe juu yetu sote. Na moto wa Roho Mtakatifu uje juu yetu. Na nguvu za ufufuo zidhihirishwe. Mungu, jinsi tunavyokushukuru, usiku huu. Sisi tu Wako. Twajitolea kwa vyo vyote Kwako, Bwana.

40 Niendapo huko, sijui wapi au vipi, au kipi nitakachofanya, nakutumainia Wewe, Mwenyezi Mungu, kwamba utaniongoza, mtumishi Wako asiyefaa, ili nitumiwe kwa heshima na kwa utukufu wa Mwenyezi. Tujalie hayo, Baba.

41 Pokea maombi yetu. Bariki juhudi zetu. Ponya wagonjwa na wanaoteseka, kiroho na kumwili pia. Na utufanye watumishi Wako. Sisi ni udongo, Nawe u Mfinyanzi. Tufinyage, kila mmoja wetu, upendavyo Wewe, ili tuunganike pamoja na Kristo Yesu,

kama washiriki wa mwili Wake. Kwa kuwa twaomba kwa Jina la Yesu, na kwa ajili Yake na ya injili Yake. Amina na amina.

42 [Ndugu mmoja anena katika lugha. Ndugu mwingine atoa tafsiri—Mh.] Asante sana, Baba, Mungu. Twakushukuru kwa mausia haya ya huu Mwaka Mpya ambayo yatutuma nje na matumaini na faraja ya kujua kuwa kupitia kwa kunena haya maneno kwa watu hawa ambao hawakujua, kuwa Ujumbe huu ni kweli, nawe watushauri tuushikilie. Tutafanya yote tujuayo, Bwana, kukushikilia Wewe na Neno Lako.

43 Tupokee katika Jina Lake Yeye aliyetufundisha sote kuwa yatupasa kuomba hivi, [Ndugu Branham pamoja na makutano wanaomba pamoja—Mh.]: "Baba yetu uliye mbinguni, Jina Lako litukuzwe, Ufalme Wako uje, Mapenzi Yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni Wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina."

44 Bwana awabariki na kuwatunza. Lakini wale sasa ambao hawana budi kwenda nyumbani kwao. . . Sasa dakika tano zimepita, ni dakika tano katika mwaka wa '63. Sasa Mungu awabariki. Na—nanyi mnaotaka kubaki kwa ajili ya ushirika, mmekaribishwa kubaki, tutafurahia kuwa nanyi. Si ushirika wa faraghani, ni kwa kila mwamini aliye katika ushirika wa Kristo. Mwakaribishwa kuketi na kupokea ushirika pamoja nasi. Na sababu ya kufanya hivyo ni kwamba hili ndilo jambo la kwanza, tunaanza safari. Na Israeli, kabla hawajaanza safari yao, walichinja mwana-kondoo na kula mboga chungu, na kuanza safari yao. Nami niliwaza, "Hili lafaa jinsi gani usiku huu!" Mwana-kondoo amechinjwa, ametayarishwa, ile karamu, na ni iku wa manane. Hapa ndipo walipomla, mwajua, usiku wa manane. Kwa hivyo hebu nasi. Ninyi mnaotaka kubaki nasi na kujitayarisha kwa safari ijayo, iliyoko mbele, tutafurahia kuwa nanyi. Mungu awabariki.

45 Na ninyi ambao hamna budi kuondoka sasa, mwaweza kwenda nyumbani kwenu, na Mungu awe nanyi hadi nitakapokutana nanyi tena. Amina. Wengine wenu mwaweza kuketi ndiposa tuanze ushirika. Dada ata . . . Vema, bwana.

> Hata twonane huko juu,
> Hata twonane Kwake kwema; (Kwake kwema)
> Hata twonane huko juu,
> Mungu awe nanyi daima.

46 Hebu tuuimbe tena hali tukingoja, mwajua, kwa ajili ya wale wanaoondoka. Huenda ikatulia, na tena hili ni jambo lenye uchaji sana. Nitasoma kitu fulani toka kwa Maandiko hapa sasa hivi ambacho ni kizuri sana, sana, sana. Sasa hebu na tuuimbe tena.

Hata twonane! (Tusalimiane kwa mikono na mtu fulani)
(Ikiwa kuna kitu chochote kibaya maishani mwako, mtu huyo uliyemkosea yuko hapa, mwendee na msameheane.)
Hata twoanane huko juu!
Mungu . . . (mpiga kinanda aweza kuja kwenye kinanda?) . . . nanyi daima!

Hata twonane huko juu,
Hata twonane kwake kwema;
Hata twonane huko juu,
Mungu awe nanyi daima.

Yeye akulinda,
Yeye akulinda;
Kupitia nuruni au uvulini,
Yeye akulinda.

47 Hebu tuuimbe tena.

Yeye akulinda,
Yeye akulinda;
Kupitia nuruni au uvulini,
Yeye akulinda.

48 Huo sio mzuri? Hebu tuimbe tena wanapotulia.

Yeye . . . (fungeni macho yenu) . . . akulinda,
Yeye akulinda,
Kupitia nuruni au uvulini,
Yeye akulinda.

49 Baba wa Mbinguni, tuna furaha zaidi kuwa tumegundua kwamba hilo ni kweli, katika wakati wetu ulio na giza zaidi au kupitia katika nuru, Yeye hatupungukii wala kutukana. Tuna furaha kwa hilo kuwa tunalo, tumaini letu halijajengwa kwa chochote ila juu ya Damu Yake Yesu na haki Yake. Twatumaini, Bwana, si sifa za ulimwengu huu. Twatumaini! Hatuthubutu kutegemea mwili, hata uwe mzuri vipi, bali tunategemea kabisa Jina la Yesu. Jinsi tunavyokushukuru, Baba.

50 Sasa twakaribia kushiriki katika mojawapo wa ile—mojawapo ya maagizo ya kawaida uliyotuachia. Mojawayo ni ubatizo, nyingine ni ushirika, na inayoifuata ni kutawadhana miguu. Ee Mungu, twaingia kwa unyenyekevu, tukijua kuwa huyu Mwana-Kondoo ni Mwana-Kondoo wa pasaka. Ile—ile safari ndefu ya jangwani ilikuwa tu mbele ya watoto hao. Ile damu lazima iwekwe kwanza kwenye kizingiti cha mlango, kabla mwana-kondoo wa pasaka hajaliwa.

51 Mungu, chunguza mioyo yetu sasa. Je, ile Damu iko humo Bwana? Kama haimo, twaomba kuwa—kuwa utaiweka sasa hivi, ukiondoa dhambi zetu na kuzifunika, nazo zitatengwa nasi, Bwana, dhambi za ulimwengu huu, ili tuwe watakatifu na wa

kupendeza mbele za Baba yetu sasa tunapokuja kula ule—ule mwili wa Damu iliyomwagwa ya Mwana-Kondoo wetu, Mwana wa Mungu, Mwokozi wetu. Chunguza mioyo yetu tunaposoma, Baba, na ndipo utufanye tuwe Wako Wewe. Kwa kuwa twaomba katika Jina la Mwana-Kondoo, Yesu Kristo. Amina.

52 Katika Kitabu cha—cha Wakorintho, sura ya 11, nataka kusoma vifungu vichache, kuanzia kifungu cha 23 nasoma haya. Ni Paulo akinena na kanisa la Wakorintho.

> *Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule. . .aliotolewa alitwaa mkate,*
>
> *Naye akisha kushukuru akaumega, akasema, Twaeni mle: huu ndio mwili Wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho Wangu.*
>
> *Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe,* akasema, lakini baada ya kula. . .(samahani, hebu nirudie tena.)
>
> *Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, kikombe hiki ni agano jipya katika damu Yangu; fanyeni hivi kwa ukumbusho, kila mnywapo, kwa ukumbusho Wangu.*
>
> *Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.*
>
> *Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana.*
>
> *Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe.*
>
> *Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili.*
>
> *Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi, na dhaifu, na. . .watu kadha wamelala.*
>
> *Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa.*
>
> *lla tuhukumiwapo, twarudiwa na Bwana, isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia.*
>
> *Kwa hivyo, ndugu zangu, mkutanikapo mpate kula, mngojane;*
>
> *Mtu akiwa na njaa, na ale nyumbani kwake; msipate kukutanika kwa hukumu. Na hayo yaliyosalia nijapo nitayatengeneza.*

53 Na waza kuhusu huu, kuwa wakati wa kicho sana! Imeandikwa pia kuwa wakati hii meza ya Bwana ilipoandaliwa kwa mara ya kwanza, na kutawadhana miguu. . .ambako hatutafanya usiku huu, kwa sababu hatuna maji. Maji yote

yamekatwa na hatukuwa hata na vifaa vya mahali pa haja usiku huu, kwa sababu iliwabidi kuyaunganisha pamoja vizuri walivyoweza ili tuwe na ibada hii usiku huu. Lakini tutafanya jinsi walivyofanya, inasema, naamini Luka alilieleza, kuwa, "Walipokwisha kuimba, wakatoka nje." Lakini wajua hilo linachowakulisha? Je, mwajua, mwanzoni, wakati hili agizo lilipopewa Israeli, huko Misri, walikuwa njiani kuelekea nchi ya ahadi. Na hivyo ndivyo tujisikiavyo usiku huu, kuwa tumo njiani kwenda Nchi ya Ahadi. Na safari hiyo iko mbele yetu.

54 Nao walikuwa na ishara, kusudi malaika wa mauti alipopita, basi kungekuwa na damu mlangoni, la sivyo, mwana wa kwanza au mtoto wa kwanza angekufa katika nyumba hiyo. Wazo lilikuwa, na maana yake halisi ilikuwa, kwanza weka damu. Je, mlitambua jinsi Paulo alivyoiweka hapa? "Mtu yeyote akila isivyostahili, yeye hula na kunywa hukumu yake, kwa kutokuupambanua mwili wa Bwana," ambayo yamaanisha kitu kile kile, hayo mauti, mauti ya kiroho, inakalia juu ya mtu ambaye anashiriki meza ya Bwana isivyostahili. Hilo lingekuwa, kunywa pombe na kuendelea kutenda yasiyofaa, na kuishi kama ulimwengu, na kuja katika meza ya Bwana. Haitupasi kufanya hivyo. Sasa hebu tuoshe mioyo yetu na kuosha mikono yetu kwa. . .na mawazo yetu toka kwa mawazo maovu, tupate kuja katika meza ya Bwana, kwa unyenyekevu na utakatifu, kwa maana tunajua kuwa tunajiunganisha pamoja na Dhabihu yetu, Yesu Kristo, ambaye ndiye wokovu pekee.

55 Na sasa, usiku huu, jinsi tutakavyofanya hili, ni mmoja wa wazee asimame hapa, Ndugu Zabel. Nami nafikiri, Ndugu Zabel, usiku huu, kama ungeitana toka kwenye jukwaa kwanza, ili watu hawa waje wautunge mstari wako wa kwanza hapa jukwaani, ukipenda. Sasa, Ndugu Zabel atawaongoza katika dakika chache, mara tu tunapobariki ushirika huu.

56 Na huu mkate wa kosher, uliookwa na Mkristo, haujatiwa chachu. Na mkiutazama, mkiuweka mdomoni, si laini, ni kama kuwa mchungu. Ulikunjwa-kunjwa na kuvunjwa, ulioungamanishwa, hilo lamaanisha mwili wa Bwana Yesu uliovunjwa, ukaungamanishwa. Lo, ninapowaza hili, moyo wangu waonekana kama unaruka pigo moja! Ninapowaza kuwa Yeye aliungamanishwa na kujeruhiwa na kupigwa, Mwana wa Mungu asiye na hatia! Je, wajua sababu Yeye akafanya hivyo? Kwa sababu mimi nilikuwa na hatia. Naye akawa mimi, mwenye dhambi, ili mimi kwa dhabihu Yake niweze kufananishwa Naye, Mwana wa Mungu. Ni Dhabihu jinsi gani!

57 Na tuinamishe vichwa vyetu. Mungu Mtakatifu Sana, kwamba nashika katika sahani hii ya chuma usiku huu, huu mkate unaowakilisha mwili wa Bwana uliovunjwa, ukaungamanishwa, ukachubuliwa, ukapigwa, wakati huyo nabii alipopaza sauti, "Alijeruhiwa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa ajili ya maovu yetu, adhabu ya amani yetu

ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Lo, jinsi tunavyokumbuka hilo, Bwana! Ninapojifungamanisha kwa hiyo dhabihu usiku huu, na makutano hawa vivyo hivyo pia, Bwana, katika Dhabihu, na tukumbuke Bwana wetu, mauti Yake na mapigo Yake, na yale yote aliyoyapitia kwa ajili yetu, tunapokula mkate huu kwa vinywa vyetu. Mungu, sisi tu watu wasiostahili. Hatufai kwa kitu kitakatifu kama hiki, kwa hivyo ruhusu utakatifu Wako, Bwana, Uwepo Wako na Damu Yako, vioshe mioyo yetu. Na tunapoupokea na tukusudie akilini mwetu kumtumikia Yeye mchana na usiku, siku zote za maisha yetu. Sasa, takasa mkate huu kwa matumizi yake. Twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

58 Nami nimeshikilia hiki mkononi mwangu kwa miaka thelathini. . . yapata miaka thelathini na mitatu ya huduma niliyomtumikia Bwana Wangu, na mimi—nami najionea aibu. Lakini nawaza, ningef anyaje kama ningalikuwa na matone mawili ya Damu Yake halisi mkononi mwangu usiku huu? Ningef anyaje nayo? Lakini, mwajua, nimekuwa nalo mkononi mwangu usiku huu, machoni Pake, iliyo kuu zaidi, ununuzi wa damu Yake, Kanisa Lake. Kwa hivyo nishikapo hiki, na maji haya ya hizi zabibu, nawaza kuhusu hilo. Yeye alisema, "Sitakunywa tena kabisa uzao wa mzabibu hata siku ile nitakapounywa mpya pamoja nanyi katika Ufalme wa Baba Yangu." Ndipo tazama kuwa baada ya vita vya dhambi kuisha, kitu cha kwanza tutakachofanya mara tu tutakapofika kule ng'ambo ya pili ni kushiriki ushirika, ile meza ya Bwana.

59 Na hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa tunapobariki hii divai. Baba yetu uliye Mbinguni, ninapowaza, ninaposhika hii divai hapa ambayo inawakilisha Damu ya Yesu, jinsi kwamba katika Damu hiyo inayotiririka dhambi zangu zimeondolewa. Zimewekwa katika bahari ya usahaulifu, na hazitakumbukwa tena. Na kwa hii Damu, siku moja mvulana aliyekuwa akifa alilala huko hospitalini, Nawe uliniokoa. Ee Mungu, jinsi ninavyokushukuru, Bwana. Ndiposa ukanipa agizo katika Roho Mtakatifu, kuwaongoza watu hadi Kalvari na niwaonyeshe njia ya kwenda Nyumbani. Asante, Baba. Na sasa takasa hii divai kwa matumizi iliyokusudiwa. Na kila mtu ashirikiye katika sakramenti hii, usiku huu, apokee nguvu za kiroho na za kimwili kwa ajili ya safari iliyoko mbele. Kwa kuwa twomba katika Jina la Yesu. Amina.

60 [Mkutano unahudumiwa ushirika. Nafasi tupu katika ukanda—Mh.] Kusimama hapa na kuwaangalia jamaa wakiingia, na hivyo ndivyo itakavyokuwa hivi karibuni, jamaa kwa jamaa, na safu kwa safu, kundi kwa kundi, mmoja kwa mmoja. Tutakapomlaki, utakuwa wakati wa jinsi gani, wakati hawa wanadamu wote waliokuwa juu ya nchi, ambao walimwamini Yeye na kumtumaini, watakutana hapo siku hiyo. Je, si litakuwa la ajabu?

61 Hatutatawadhana miguu usiku huu kwa sababu ya maji. Hatuna vifaa vya kutosha sasa hivi, na vitawekwa hivi karibuni, twatumaini. Wao wanaendelea vema, kujenga haraka jengo jipya la ibada. Ingawaje nadhani yafaa sana kuwa na ushirika tarehe moja ya mwaka hivi, wakati kama huu wa siku.

62 Sasa, ninyi mtokao nje ya mji, endesheni kwa makini sana kesho muendapo nyumbani. Mungu awe nanyi. Nanyi mlio wenyeji wa hapa, humu karibu, Mungu atakuwa pamoja nanyi na atawasaidia. Na sasa, Bwana akipenda, na yanibidi niondoke kwa ajili ya mkutano unaofuata utakaokuwa huko Arizona, na kisha Mungu akipenda, nitarudi tena kuwa nanyi kwa ajili zile *Mihuri Saba,* kama vile tu nilivyoahidi. Bila shaka nahitaji maombi yenu. Nawatakeni mfanye hivyo sana, kwa hivyo msisahau kuniombea. Na kila kitu kiendelee vyema kwenu. Nami bila shaka nimekuthamini kuhudhuria kwenu na jinsi mmesikiza yale nimesema katika Injili. Naamini kuwa tunafanya badiliko sasa. Nami na—nawashukuru kwa ukarimu wenu.

63 Na wengi wenu wameendesha motakaa maili nyingi waje kusikiza mtu hivi hitu kama mimi nikijaribu kuleta Neno la Mungu. Nina hakika ni kitu fulani zaidi ya hicho—hicho ndicho mlichokuja kusikia zaidi yangu, kwa sababu sina chochote ambacho ningetoa. Sina elimu, si mtu mashuhuri, hamna kitu kwangu. Ndipo nionapo watu wakiendesha magari maili mia kadha na kusimama wakingoja hapa, saa nane usiku, haikuwa kwa sababu ya nilichokuwa nacho. Ni Kristo. Nafurahi sana mwampenda. Nami pia nampenda. Nasi sote pamoja twampenda. Na kwa sababu twampenda, haitatubidi kuachama. Twaweza kutengana kidogo hapa na pale, wakati unapoendelea, lakini tutakuwa pamoja tena. Imekuwa shauku yangu kujaribu kuongoza watu hadi mahali hapo.

64 Na sasa kuanzia mwaka mpya, nataka kusema, si "Mwaka Mpya wa Furaha," kwenu, nataka kuwaambieni hili, "Mungu awabariki." Naye akifanya hivyo, hilo ndilo pekee tunalohitaji kwa mwaka ujao. Nami natumaini Yeye atatubariki.

65 Na sasa kwa neema Yake, tutajaribu mwaka huu ujao, akiniweka hai, na kuwawekeni hai, kwa neema Yake natumaini nitakuwa mchungaji mzuri zaidi mwaka ujao kuliko nilivyokuwa mwaka huu, natumaini nitakuwa mtumishi bora kwa Kristo. Nitajitahidi sana niishi karibu zaidi, mwaminifu zaidi, niulete Ujumbe kama tu Yeye anavyonipa, nitauleta kwenu vema niwezavyo, bila kuwanyima cho chote Yeye atakachonipa mimi niwape. Nitafanya chote nijuacho. Nami najua mwajisikia vivyo hivyo. Nanyi, mwajisikia vivyo hivyo kwamba sote twataka kufanya kazi pomoja sasa, kwa kuwa nuru za jioni hakika zinafifia na jua linatua kwa mbali. Nchi inapoa, twajua hilo, tukinena kiroho, kanisa linapoa na ufufuo umekwisha. Hatujui kipi kitakachofuata, lakini tutamtumainia

Mungu kwa hayo, cho chote kile. Na sasa kama sisi wakati mwingine. . .

66 Nataka mkumbuke kuwa Maskani haya hapa yana mmojawapo wa wachungaji wazuri zaidi waliomo duniani, Ndugu Orman Neville, mcha Mungu, mtu mzuri. Na nisipokuwepo, Ndugu Neville ndiye anayesimamia yote, kama tu vile mimi ningekuwako hapa. Wadhamini, Mashemasi, na wengineo, lazima wadumu katika huduma zao kama vile wao wafanyavyo. Na haya ndiyo makao yetu makuu. Hapa ndipo penye tuta. . .penye tunakaa papa hapa. Billy Paul hatakuwa nami kule nje, ni kwa ule mkutano tu, yeye atarudi hapa. Shughuli na kadhalika zitaendezwa kutoka hapa vivyo vivyo. Kuenda tu kule, hilo si kuonyesha kuwa ninawaacha. Ninaenda tu, mwaelewa, ni ono tu. Sijui maana yake. Natumaini na kuamini kuwa itakuwa kwa manufaa ya Kanisa lote. Nami najua itakuwa bora kwetu sisi sote tukifuata uongozi wa Bwana. Hilo ndilo lote tujualo kutenda. Si rahisi kwangu. Nakumbuka wakati mmoja hapo mbeleni ilinilazimu kuondoka kanisani hapa. Baadhi yenu ninyi watu wa zamani mwakumbuka hilo, jinsi singeweza kulifanya! Nawapenda watu.

67 Nilipokuwa mvulana mdogo sikupendwa, hakuna ye yote aliyenijali nilipokuwa mtoto, nami, nilipompata mtu fulani aliyenipenda, ni—"ningelitaka kuwafia." Na sasa, kwa sababu mtu fulani anakupenda, mtu fulani anakujali. Nilikuwa nikipanda siku moja juu ya kikingi na kulabu yangu ikatereza toka kwenye kikuukuu cha mwerezi, na kifundo kilikuwa juu sana, nami nikakigonga kwa chombo changu cha kujishikilia na nikapinduka, na kuanguka umbali upatao futi kumi na tano na kushika mkono wangu. Mwanamke mmoja akapiga mayowe, naye akajipapasa—papasa mwenyewe hivi. Kila mara nilimpenda mwanamke huyo, yeye alijali. Yeye alikuwa mtu aliyejali. Nami kila siku niliwaza, "wowote wanijalio nawapenda."

68 Na hapa wakati fulani uliopita nalipotelemka mjini, nalikuwa nawaza kuhusu siku zilizopita, na kile Mungu amenitendea, nami hakika nashukuru. Nami nawashukuru kwa ajili ya upendo wenu na ushirika. Nami singejaribu kamwe kuwaongozeni vibaya. Kila mara itakuwa kwa njia sahihi, vizuri nijuavyo. Nanyi mwanishuhudia, sikusema cho chote kunihusu mimi, kila mara imekuwa Yesu Kristo. Mwaona? Mwaona? Nimejaribu kusimama karibu sana na Neno Lake kama nijuavyo kusimama, kuwaongozeni ninyi na kuwarejesha ninyi hadi mahali hapa.

69 Nami nawakabidhi ninyi mikononi mwa Ndugu Neville, kwanza katika mikono ya Mungu, na ndipo katika mkono na ulizi wa Ndugu Neville, kuchunga hili kanisa na kutunza huu urithi hadi nitakapokuwa na huu mkutano na nirudi kwenu tena. Nikitumaini kuwa ifikapo wakati huo nitaweza kuwaletea

ufunuo mkuu toka kwa Mungu, utakaofurahisha kila moyo na kulitukuza Kanisa la Mungu.

70 Sisi kila mara hupokea ushirika. Sitaki kusema lingine zaidi, mwajua jinsi ninavyojisikia. Nami nadhani wimbo utapasao kuimba sasa, *Yesu kwa Imani, Nakutumaini.* Na tunaposimama na kuuimba, hebu tusalimiane kwa mikono, na kusema "Mungu akubariki."

> Yesu kwa imani,
>
> Pekee Yako;
> Nisikie sasa,
> Na kunitakasa,
>
> Tangu leo.

71 Sasa hebu tumwinulie mikono.

> Yesu kwa imani,
> Nakutumaini,
> Pekee Yako;
> Nisikie sasa,
> Na kunitakasa,
> Ni Wako kabisa
> Tangu leo.

72 Hata twonane! Hebu tuimbe Hata Twaonane Huko Juu. Kila mtu aimbe.

> Hata twonane huko juu,
> Hata twonane Kwake kwema;
> Hata twonane huko juu,
> Mungu awe nanyi daima!
>
> Hata twonane huko juu,
> Hata twonane Kwake kwema; (Kwake kwema)
> Hata twonane huko juu,
> Mungu awe nanyi daima!

73 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa, Ndugu Neville, mbona usituruhusu twende kwa kutuombea. Mungu awabariki.

Lile Shindano SWA62-1231
(The Contest)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatatu jioni, Desemba 31, 1962, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org